

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA NISHATI

**BARAZA LA USHAURI LA WATUMIAJI WA HUDUMA ZA
NISHATI NA MAJI (EWURA CCC)**



**MAONI YA BARAZA LA USHAURI LA WATUMIAJI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI
(EWURA CCC) JUU YA OMBI LA MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA
ROMBO LA MAPITIO YA BEI ZA HUDUMA ZA MAJI KWA KIPINDI CHA MIAKA MITANO
KUANZIA 2026/27–2030/31**

1. Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA Consumer Consultative Council – EWURA CCC) linapenda kuwasilisha maoni yake kuhusu ombi la Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Rombo (Rombo WSSA) la kutaka kuidhinishiwa mapitio ya bei za huduma za maji kwa kipindi cha miaka mitano, kuanzia mwaka wa fedha 2026/27 hadi 2030/31.

Maoni haya yametokana na mapitio ya nyaraka zilizowasilishwa na Rombo WSSA, zikiwemo:

- i. Ombi la Mapitio ya Bei (Tariff Review Application);
- ii. Mpango Biashara wa miaka mitano 2026/27–2030/31 (Business Plan);
- iii. Taarifa za Fedha zilizokaguliwa;
- iv. Azimio la Bodi kuhusu Ombi la Mapitio ya Bei;
- v. Muhtasari wa Kikao cha Wadau; na
- vi. Kanuni za EWURA za Maombi na Uwekaji wa Bei za Huduma za Maji za mwaka 2020 (EWURA Water Tariff Application and Rate Setting Rules, 2020).

2. Katika mapitio ya Ombi la Mapitio ya Bei pamoja na Mpango Biashara wa Rombo WSSA, Baraza limebaini kutokuwiana kwa taarifa kuhusu wastani wa bei ya maji inayopendekezwa kwa mwaka wa fedha 2026/27. Fomu Na. 1 ya Ombi la Mapitio ya Bei inaonesha wastani wa bei ya sasa kuwa Shilingi 900 kwa mita ya ujazo, huku wastani wa bei unaopendekezwa kwa mwaka 2026/27 ukiwa Shilingi 1,000 kwa mita ya ujazo (Tariff Application, Form 1, uk. 4). Kwa msingi huo, ongezeko linaloonekana katika Fomu hiyo ni takribani asilimia 11.1.

Hata hivyo, Mpango Biashara unaonesha wastani wa bei unaopendekezwa kwa mwaka 2026/27 kuwa Shilingi 1,217.71 kwa mita ya ujazo. Kiwango hicho kinaendana na makadirio ya mahitaji ya mapato yatokanayo na mauzo ya maji ya Shilingi 4,609,580,000, yakigawanywa kwa kiasi cha maji kinachotarajiwa kutozwa bili cha mita za ujazo 3,785,448.78 katika mwaka huo (Business Plan, Executive Summary, uk. ix; Jedwali Na. 22, uk. 60).

Kwa kutumia kiwango hicho, wastani wa bei ungeongezeka kutoka Shilingi 900 hadi Shilingi 1,217.71 kwa mita ya ujazo, sawa na ongezeko la takribani asilimia 35.3, badala ya asilimia 11.1 inayoonekana endapo kiwango cha Shilingi 1,000 kilichoainishwa katika Fomu Na. 1 kitatumika.

Baraza linaona kuwa tofauti hiyo ni muhimu kwa sababu Fomu Na. 1 ndiyo sehemu ya Ombi la Mapitio ya Bei inayoainisha viwango vinavyoombewa idhini, wakati kiwango cha Shilingi 1,217.71 kinaonekana kuwa ndicho kinachotokana na mahitaji ya mapato na kiasi cha maji kinachotarajiwa kutozwa bili. Bila taarifa hizo kuoanishwa, inakuwa vigumu kubaini kwa uwazi kiwango halisi cha wastani wa bei kinachoombewa idhini kwa mwaka 2026/27 na kutathmini kwa usahihi athari yake kwa watumiaji.

Aidha, tofauti kati ya ongezeko la asilimia 11.1 na asilimia 35.3 ni kubwa kiasi cha kuathiri tathmini ya uwezo wa watumiaji kumudu huduma pamoja na tathmini ya mahitaji ya mapato yanayotarajiwa kurejeshwa kupitia bei.

Kutokana na hali hiyo, Baraza linaishauri EWURA:

- i. Kujiridhisha kuhusu kiwango halisi cha wastani wa bei kinachoombewa idhini kwa mwaka 2026/27 kati ya Shilingi 1,000 na Shilingi 1,217.71 kwa mita ya ujazo;
- ii. Kuitaka Rombo WSSA kuoanisha taarifa za bei katika Fomu Na. 1 ya Ombi la Mapitio ya Bei, Mpango Biashara na makadirio ya mahitaji ya mapato ili nyaraka zote zitumie msingi mmoja wa bei;
- iii. Kujiridhisha kuwa kiwango kitakachotumika katika kufanya uamuzi wa bei kinaendana na mahitaji ya mapato yaliyothibitishwa pamoja na kiasi cha maji kinachotarajiwa kutozwa bili; na
- iv. Kuhakikisha kuwa athari ya bei kwa watumiaji inatathminiwa kwa kutumia kiwango halisi kitakachoidhinishwa, ili kiwango cha ongezeko na uwezo wa watumiaji kumudu huduma viweze kupimwa kwa usahihi.

3. Mpango Biashara wa Rombo WSSA unaonesha kuwa wastani wa bei ya maji inayotokana na mahitaji ya mapato unatarajiwa kubadilika kwa kiasi kikubwa katika kipindi cha miaka mitano cha mapitio ya bei. Wastani huo unakadiriwa kuwa Shilingi 1,217.71 kwa mita ya ujazo mwaka 2026/27, na kuongezeka hadi Shilingi 1,795.59 mwaka 2027/28, Shilingi 1,930.28 mwaka 2028/29, Shilingi 1,986.14 mwaka 2029/30, kabla ya kushuka kidogo hadi Shilingi 1,980.79 mwaka 2030/31 (Business Plan, Executive Summary, uk. ix; Jedwali Na. 22, uk. 60).

Mwenendo huo unaonesha kuwa, kwa kutumia kiwango cha Shilingi 1,217.71 kama wastani wa bei wa mwaka 2026/27, wastani wa bei unaongezeka kwa takribani asilimia 47.5 katika mwaka unaofuata wa 2027/28. Aidha, ikilinganishwa na wastani wa bei ya sasa wa Shilingi 900 kwa mita ya ujazo, wastani wa Shilingi 1,795.59 unaokadiriwa kwa mwaka 2027/28 ni takribani asilimia 99.5 zaidi ya kiwango cha sasa.

Baraza limebaini kuwa ongezeko hilo linaendana na kuongezeka kwa mahitaji ya mapato yatokanayo na mauzo ya maji kutoka takribani Shilingi bilioni 4.610 mwaka 2026/27 hadi Shilingi bilioni 7.477 mwaka 2027/28, sawa na ongezeko la takribani asilimia 62.2. Katika kipindi hicho, kiasi cha maji kinachotarajiwa kutozwa bili kinaongezeka kutoka takribani mita za ujazo milioni 3.785 hadi milioni 4.164, sawa na ongezeko la takribani asilimia 10 (Business Plan, Jedwali Na. 22, uk. 60).

Aidha, Jedwali Na. 22 linaonesha kuwa katika kipindi hicho gharama za uendeshaji na matengenezo zinaongezeka kutoka takribani Shilingi bilioni 3.258 hadi Shilingi bilioni 4.685, huku marejesho ya uwekezaji yakiongezeka kutoka takribani Shilingi bilioni 1.772 hadi Shilingi bilioni 2.389. Wakati huohuo, kiasi kinachopunguzwa kwenye mahitaji ya mapato kama Idle Fund from Investment kinapungua kutoka takribani Shilingi bilioni 1.380 hadi Shilingi milioni 690.323.

Baraza linatambua kuwa Mamlaka inahitaji mapato ya kutosha kugharamia uendeshaji na matengenezo ya miundombinu, kuongeza uzalishaji na kuhakikisha uendeleu wa huduma. Hata hivyo, kwa kuwa sehemu kubwa ya mahitaji hayo ya mapato inatarajiwa kurejeshwa kupitia bei ya maji, ongezeko kubwa la bei ndani ya kipindi kifupi linahitaji kuangaliwa pia kwa kuzingatia uwezo wa watumiaji kumudu huduma na kiwango cha maboresho ya huduma watakayopata kutokana na ongezeko hilo.

Umuhimu wa jambo hili unaongezeka zaidi kwa kuzingatia hali ya sasa ya huduma. Mpango Biashara unaonesha wastani wa muda wa upatikanaji wa maji kwa mwaka 2025/26 kuwa takribani saa 6.93 kwa siku, huku Mamlaka ikilenga kuongeza muda huo hatua kwa hatua hadi takribani saa 21.68 kwa siku mwaka 2030/31 (Business Plan, Appendix B-3, uk. 83).

Baraza linaona kuwa malengo hayo ya kuboresha huduma ni muhimu. Hata hivyo, ongezeko la bei linapaswa kuambatana na maboresho yanayoonekana na yanayopimika katika huduma anayopokea mtumiaji. Mafanikio ya bei mpya hayapaswi kupimwa kwa ongezeko la mapato ya Mamlaka pekee, bali pia kwa kuongezeka kwa muda wa

upatikanaji wa maji, uhakika wa huduma, kupungua kwa maji yasiyoingiza mapato na kuongezeka kwa idadi ya wananchi wanaopata huduma.

Kutokana na hali hiyo, Baraza linaishauri EWURA:

- i. Kufanya tathmini ya kina ya ongezeko la bei linalopendekezwa katika kipindi cha miaka mitano, hususan ongezeko la takribani asilimia 47.5 kati ya mwaka 2026/27 na 2027/28, na kujiridhisha kuhusu vipengele vya gharama na mahitaji ya mapato vinavyolisababisha;
 - ii. Kujiridhisha kuwa gharama zinazochangia ongezeko la mahitaji ya mapato na hatimaye bei ni za lazima, zina ufanisi na zinahusiana moja kwa moja na utoaji na uboreshaji wa huduma;
 - iii. Kuzingatia uwezo wa watumiaji kumudu huduma wakati wa kufanya uamuzi kuhusu viwango vya bei vinavyopendekezwa, hususan kutokana na ukubwa wa ongezeko linalotarajiwa katika miaka ya mwanzo ya utekelezaji;
 - iv. Kuhakikisha kuwa ongezeko la bei linaambatana na malengo ya kila mwaka yanayopimika ya maboresho ya huduma, ikiwemo muda wa upatikanaji wa maji, kupungua kwa maji yasiyoingiza mapato, kuongezeka kwa uzalishaji na idadi ya wananchi wanaopata huduma; na
 - v. Kufuatilia utekelezaji wa malengo hayo katika kipindi chote cha uhalali wa bei ili kuhakikisha kuwa ongezeko la gharama linalobebwa na watumiaji linaendana na maboresho halisi ya huduma wanazopokea.
4. Mpango Biashara wa Rombo WSSA unaonesha kuwa kiwango kikubwa cha maji yasiyoingiza mapato (Non-Revenue Water – NRW) ni mojawapo ya changamoto kuu za kiutendaji zinazokabili Mamlaka. Rombo WSSA imeweka lengo la kupunguza NRW kutoka asilimia 67.64 hadi asilimia 25 ifikapo Juni 2031 (Business Plan, Executive Summary, uk. viii; Jedwali Na. 19, uk. 39).

Mpango Biashara unaeleza kuwa kiwango kikubwa cha NRW ni tatizo kubwa kwa Mamlaka na kinahusishwa, pamoja na mambo mengine, na uwepo wa wateja wanaotozwa kwa makadirio bila mita, miundombinu ya maji iliyochakaa, miunganisho yasiyo halali pamoja na mita za maji zilizochakaa. Hali hiyo inaelezwa kusababisha upotevu mkubwa wa mapato ya Mamlaka (Business Plan, Jedwali Na. 18, uk. 38).

Katika makadirio yaliyotumika kukokotoa bei, Rombo WSSA inatarajia kupunguza NRW hatua kwa hatua kutoka asilimia 50 mwaka 2026/27 hadi asilimia 45 mwaka 2027/28, asilimia 38 mwaka 2028/29, asilimia 30 mwaka 2029/30 na asilimia 25 mwaka 2030/31. Kwa mwaka 2026/27, Mamlaka inakadiria kuzalisha takribani mita za ujazo milioni 7.571, lakini kutokana na kiwango cha NRW cha asilimia 50, kiasi kinachotarajiwa kutozwa bili ni takribani mita za ujazo milioni 3.785. Kiasi hicho ndicho kimetumika pamoja na mahitaji ya mapato yatokanayo na mauzo ya maji katika kukokotoa wastani wa bei wa Shilingi 1,217.71 kwa mita ya ujazo.

Baraza linaona kuwa kupunguza NRW kuna umuhimu wa moja kwa moja kwa watumiaji na uendeleu wa kifedha wa Mamlaka. Kiwango kikubwa cha maji yanayozalishwa lakini yasiyoweza kutozwa bili kutokana na uvujaji, hitilafu za mita, miunganisho yasiyo halali au sababu nyingine hupunguza kiasi cha maji kinachoweza kuuzwa ambacho ndicho msingi wa kurejesha mahitaji ya mapato kupitia bei. Kwa hiyo, kuongeza ufanisi katika usimamizi wa maji yanayozalishwa kunaweza kuongeza kiasi cha maji kinachotozwa bili na kupunguza shinikizo la gharama kwa kila mita ya ujazo inayouzwa.

Baraza linatambua kuwa Rombo WSSA imeweka hatua mahsusi za kukabiliana na tatizo hilo. Jedwali Na. 19 la Mpango Biashara linaainisha, pamoja na hatua nyingine, kuongeza uwiano wa wateja wenye mita kutoka asilimia 96 hadi asilimia 100; kufunga mita 6,130 kwa wateja wanaotozwa kwa makadirio na mita 15,113 kwa wateja wapya; kufunga mita 1,350 za malipo kabla; kufanya ukaguzi wa miunganisho isiyo halali; kuhamisha takribani mita 6,000 za wateja katika maeneo yanayofaa; kuanzisha maeneo sita ya kupima na kudhibiti mtiririko wa maji katika mtandao (District Metered Areas – DMAs); pamoja na kubadilisha mita 9,000 zilizoharibika au zilizochakaa (Business Plan, Jedwali Na. 19, uk. 39).

Aidha, Mpango Kazi unaonesha kuwa baadhi ya hatua hizo zimetengewa rasilimali na muda wa utekelezaji katika kipindi cha Mpango Biashara, ikiwemo ununuzi na ufungaji wa mita kwa wateja wanaotozwa kwa makadirio na wateja wapya, mita za malipo kabla, pamoja na shughuli za kudhibiti miunganisho isiyo halali na uvujaji wa maji.

Baraza linaunga mkono hatua hizo kwa kuwa zinaweza kuongeza ufanisi wa mfumo na kiasi cha maji kinachoweza kuwafikia watumiaji na kutozwa bili. Hata hivyo, kwa kuwa makadirio ya bei yenyewe yamejengwa kwa dhana ya kupungua kwa NRW kwa kila mwaka, utekelezaji na matokeo ya hatua hizo yanapaswa kuwa sehemu muhimu ya ufuatiliaji wa bei itakayoidhinishwa. Endapo malengo ya kupunguza NRW hayatatekelezwa kama ilivyopangwa, kiasi cha maji kinachoweza kutozwa bili kinaweza kuwa chini ya makadirio, jambo ambalo linaweza kuathiri mapato ya Mamlaka na kuongeza shinikizo la gharama kwa watumiaji.

Kutokana na hali hiyo, Baraza linaishauri EWURA:

- i. Kuhakikisha kuwa utekelezaji wa bei itakayoidhinishwa unaambatana na malengo ya kila mwaka ya kupunguza NRW kutoka asilimia 50 mwaka 2026/27 hadi asilimia 25 mwaka 2030/31, kama yalivyotumika katika makadirio ya bei;
- ii. Kufuatilia utekelezaji wa hatua mahsusi zilizowekwa na Rombo WSSA za kupunguza NRW, ikiwemo ufungaji na ubadilishaji wa mita, udhibiti wa miunganisho isiyo halali, ukarabati wa miundombinu, udhibiti wa uvujaji na uanzishaji wa maeneo ya kupima na kudhibiti mtiririko wa maji katika mtandao;
- iii. Kujiridhisha kuwa makadirio ya kiasi cha maji kitakachotozwa bili na mapato yatokeanayo na mauzo ya maji yanaendana na malengo halisi na yanayoweza kutekelezeka ya kupunguza NRW;
- iv. Kuitaka Rombo WSSA kuwasilisha taarifa za utekelezaji zinazoonesha kwa kila mwaka kiwango cha NRW kilichofikiwa, hatua zilizotekelezwa, gharama zilizotumika na matokeo yaliyopatikana; na

v. Kuhakikisha kuwa maboresho ya ufanisi yatokanayo na kupungua kwa NRW yanazingatiwa katika tathmini ya utekelezaji wa bei, ili manufaa ya kuongezeka kwa kiasi cha maji kinachotozwa bili yaweze kuchangia kupunguza shinikizo la gharama kwa watumiaji na kuboresha upatikanaji wa huduma.

5. Baraza limepitia ukokotoaji wa Msingi wa Mali Unaodhibitiwa (Regulatory Asset Base – RAB) pamoja na Marejesho ya Uwekezaji (Return on Investment – ROI) uliowasilishwa na Rombo WSSA katika Fomu Na. 8 ya Ombi la Mapitio ya Bei.

Kwa mwaka 2026/27, Fomu Na. 8 inaonesha mali zisizo za muda mfupi (Non-Current Assets) zenye thamani ya Shilingi 17,420,270,821.26, mtaji wa uendeshaji (Working Capital) wa Shilingi 407,216,250.00, na ruzuku (Grants) ikiwa sifuri. Kwa msingi huo, RAB imekokotolewa kuwa Shilingi 17,827,487,071.26. Kwa kutumia WACC ya asilimia 10, Marejesho ya Uwekezaji yamekokotolewa kuwa Shilingi 1,772,349,339.67 kwa mwaka 2026/27 (Tariff Application, Form 8, uk. 25).

Fomu hiyo pia inaonesha ruzuku kuwa sifuri katika ukokotoaji wa RAB kwa miaka yote ya kipindi cha bei. Wakati huohuo, Mpango Biashara unaonesha kuwa Rombo WSSA inapanga kufanya uwekezaji wa jumla wa takribani Shilingi bilioni 44.093, ambapo takribani Shilingi bilioni 33.744 zinatarajiwa kutoka katika ruzuku za Serikali na takribani Shilingi bilioni 10.349 kutoka vyanzo vya ndani vya Mamlaka. Hivyo, takribani asilimia 76.5 ya uwekezaji uliopangwa unatarajiwa kufadhiliwa kupitia ruzuku (Business Plan, Executive Summary, uk. ix).

Aidha, Ombi la Mapitio ya Bei linaeleza kuwa Mamlaka inatarajia kupata fedha za uwekezaji kutoka Serikalini kupitia Wizara ya Maji pamoja na washirika wa maendeleo, ambazo zinatarajiwa kugharamia zaidi ya asilimia 80 ya gharama za uwekezaji (Tariff Application, Sehemu ya 16, uk. 38).

Kwa mujibu wa Kanuni za EWURA za Maombi na Uwekaji wa Bei za Huduma za Maji za mwaka 2020, Rate Base ni thamani halisi ya mali zinazodhibitiwa za Mamlaka

zinazotumika katika utoaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira. Kanuni hizo pia zinatambua ruzuku kuwa msaada wa kifedha kutoka Serikali au wafadhili kwa ajili ya kugharamia matumizi ya uendeshaji au uwekezaji.

Baraza linatambua umuhimu wa ruzuku za Serikali na washirika wa maendeleo katika kugharamia uwekezaji wa miundombinu. Ruzuku hizo zina manufaa kwa watumiaji kwa kuwa zinawezesha utekelezaji wa miradi mikubwa bila gharama yote ya uwekezaji kurejeshwa moja kwa moja kupitia bei wanazolipa watumiaji.

Hata hivyo, kwa kuwa sehemu kubwa ya uwekezaji wa Rombo WSSA inatarajiwa kufadhiliwa kupitia ruzuku, Baraza linaona umuhimu wa kutenganisha kwa uwazi mali zinazofadhiliwa kwa fedha za Mamlaka na zile zinazofadhiliwa kwa ruzuku wakati wa kukokotoa RAB na ROI. Fomu Na. 8, kama ilivyowasilishwa, inaonesha ruzuku kuwa sifuri katika kipindi chote cha bei, wakati Mpango Biashara unaonesha uwekezaji mkubwa unaotarajiwa kufadhiliwa kwa ruzuku. Nyaraka zilizofanyiwa marejeo na Baraza hazijaonesha kwa uwazi ulinganisho na uoanifu wa taarifa inayothibitisha namna mali zinazofadhiliwa kwa ruzuku zimeondolewa, au zitakavyoondolewa, katika msingi wa mali unaotumika kukokotoa marejesho ya uwekezaji.

Jambo hili lina umuhimu wa moja kwa moja kwa watumiaji kwa kuwa Marejesho ya Uwekezaji ni sehemu ya Mahitaji ya Mapato yanayorejeshwa kupitia bei. Hivyo, endapo mali iliyofadhiliwa kwa ruzuku ingeendelea kujumuishwa katika msingi unaotumika kukokotoa marejesho ya uwekezaji, kungekuwa na uwezekano wa watumiaji kubeba gharama ya marejesho juu ya mali ambayo gharama yake ya uwekezaji iligharamiwa na Serikali au mshirika wa maendeleo.

Kwa hiyo, hoja ya Baraza hapa si kwamba hali hiyo imethibitishwa kutokea, bali ni kwamba ukokotoaji uliowasilishwa unahitaji kuwekwa wazi na kuhakikiwa ili kuondoa uwezekano huo na kuhakikisha kuwa watumiaji wanabeba gharama zinazostahili pekee.

Baraza limebaini pia kuwa Fomu Na. 8 inaonesha Debt Amount kuwa sifuri, lakini Weight of Debt imeoneshwa kuwa 1.00, wakati Equity Amount imeoneshwa kuwa takribani

Shilingi bilioni 15.636 lakini Weight of Equity haijaoneshwa. Pamoja na kwamba WACC imeoneshwa kuwa asilimia 10, uwasilishaji huo inahitaji kuhakikiwa ili kuhakikisha kuwa muundo wa mtaji na ukokotoaji wa WACC na ROI umeoneshwa kwa usahihi na kwa namna inayoweza kuthibitishwa (Tariff Application, Form 8, uk. 25).

Kutokana na hali hiyo, Baraza linaishauri EWURA:

- i. Kuhakiki na kuoanisha thamani ya mali iliyotumika katika kukokotoa RAB na taarifa za mali za Rombo WSSA kabla ya kuidhinisha kiwango cha Marejesho ya Uwekezaji;
 - ii. Kuhakikisha kuwa mali zinazofadhiliwa kwa ruzuku za Serikali na washirika wa maendeleo zinatambuliwa na kutengwa ipasavyo katika msingi wa mali unaotumika kukokotoa Marejesho ya Uwekezaji, kwa mujibu wa Kanuni zinazotumika;
 - iii. Kuitaka Rombo WSSA kuwasilisha ulinganisho na uoanifu wa taarifa zinazoonesha kwa kila mwaka thamani ya mali zilizofadhiliwa kwa fedha za Mamlaka, mali zilizofadhiliwa kwa ruzuku, nyongeza za mali, uchakavu pamoja na thamani ya mali inayobaki katika RAB;
 - iv. Kuhakiki muundo wa mtaji uliowasilishwa katika Fomu Na. 8, hususan taarifa za Debt Amount, Equity Amount, Weight of Debt na Weight of Equity, na kujiridhisha kuwa WACC ya asilimia 10 na ROI inayotokana nayo zimekokotolewa kwa msingi sahihi; na
 - v. Kuhakikisha kuwa ni gharama na marejesho ya uwekezaji yanayostahili pekee ndiyo yanayojumuishwa katika Mahitaji ya Mapato na hatimaye kurejeshwa kupitia bei wanazolipa watumiaji.
6. Baraza limepitia makadirio ya gharama za uendeshaji na matengenezo (Operation and Maintenance – O&M) pamoja na Mahitaji ya Mapato (Revenue Requirements) yaliyotumika katika kukokotoa bei zinazopendekezwa na Rombo WSSA.

Mpango Biashara unaonesha kuwa gharama za O&M kabla ya uchakavu zinatarajiwa kuongezeka kutoka takribani Shilingi bilioni 2.667 mwaka 2025/26 hadi Shilingi bilioni 3.258 mwaka 2026/27, sawa na ongezeko la takribani asilimia 22.1. Gharama hizo zinaendelea kuongezeka hadi Shilingi bilioni 4.685 mwaka 2027/28, Shilingi bilioni 5.659 mwaka 2028/29, Shilingi bilioni 5.989 mwaka 2029/30, na Shilingi bilioni 6.244 mwaka 2030/31 (Business Plan, Appendix U). Hivyo, kati ya mwaka 2026/27 na 2030/31, gharama za O&M zinaongezeka kwa takribani asilimia 91.7.

Sambamba na ongezeko hilo, Jedwali Na. 22 linaonesha Mahitaji ya Mapato ya Mamlaka yakiongezeka kutoka takribani Shilingi bilioni 6.002 mwaka 2026/27 hadi Shilingi bilioni 12.431 mwaka 2030/31, sawa na ongezeko la takribani asilimia 107.1. Mahitaji hayo yanajumuisha gharama za O&M, uchakavu na Marejesho ya Uwekezaji.

Baraza linatambua kuwa ongezeko la gharama za uendeshaji katika kipindi cha miaka mitano linaweza kuchangiwa na sababu mbalimbali za msingi, ikiwemo upanuzi wa huduma, ongezeko la idadi ya wateja, ukarabati wa miundombinu, ongezeko la uzalishaji wa maji pamoja na utekelezaji wa shughuli zinazolenga kuboresha ubora na uhakika wa huduma. Mpango Biashara, kwa mfano, unatarajia kuongeza uzalishaji wa maji kutoka mita za ujazo 19,187 kwa siku hadi mita za ujazo 22,902.19 kwa siku na kuongeza idadi ya wateja kutoka 29,336 hadi 44,449 ifikapo Juni 2031.

Aidha, Mpango Biashara umetumia kiwango cha mfumuko wa bei cha asilimia 3.7 kama moja ya dhana za msingi za makadirio katika kipindi cha Mpango. Baraza halitarajii, hata hivyo, kuwa gharama za O&M ziongezeke kwa asilimia 3.7 pekee, kwa kuwa gharama zinaweza pia kuathiriwa na ongezeko la shughuli na ukubwa wa huduma. Badala yake, tofauti kubwa kati ya mfumuko wa bei uliokadiriwa na ukuaji wa baadhi ya gharama inaonesha umuhimu wa kufanya uhakiki wa kina wa vichocheo vikuu vya gharama kabla ya gharama hizo kurejeshwa kupitia bei.

Kwa mfano, Kiambatisho U cha Mpango Biashara kinaonesha kuwa gharama za umeme kwa uzalishaji wa maji zimekadiriwa kuwa takribani Shilingi milioni 75.85 mwaka 2026/27

na 2027/28, lakini zinaongezeka hadi takribani Shilingi milioni 354.88 mwaka 2028/29 na kubaki katika kiwango hicho hadi mwaka 2030/31. Gharama za kemikali nazo zinakadiriwa kuongezeka kutoka takribani Shilingi milioni 26.79 mwaka 2026/27 hadi Shilingi milioni 34.20 mwaka 2030/31 (Business Plan, Appendix U).

Baraza linaona kuwa ongezeko la gharama hizo halipaswi kutafsiriwa moja kwa moja kuwa si halali au halina ufanisi. Hata hivyo, kwa kuwa gharama za O&M ni sehemu ya msingi ya Mahitaji ya Mapato na hatimaye huathiri bei anayolipa mtumiaji, ni muhimu kwa EWURA kujiridhisha kuwa ongezeko kubwa katika vipengele mbalimbali vya gharama lina sababu zinazothibitishwa na linahusiana na shughuli halisi zinazohitajika katika utoaji na uboreshaji wa huduma.

Jambo hili lina umuhimu zaidi kwa kuzingatia kwamba kati ya mwaka 2026/27 na 2027/28 pekee, gharama za O&M zinaongezeka kutoka Shilingi bilioni 3.258 hadi Shilingi bilioni 4.685, sawa na takribani asilimia 43.8. Katika kipindi hicho hicho, kama ilivyoelezwa katika Hoja Na. 3 hapo juu, wastani wa bei unaongezeka kutoka Shilingi 1,217.71 hadi Shilingi 1,795.59 kwa mita ya ujazo.

Kwa hiyo, Baraza halipingi ongezeko la gharama linalohitajika kwa uendeleu wa huduma, bali linaona umuhimu wa kuhakikisha kuwa gharama zinazopitishwa kwa watumiaji ni za lazima, zimekadiriwa kwa uhalisia, zina ufanisi na zinaendana na maboresho ya huduma yanayotarajiwa kupatikana.

Kutokana na hali hiyo, Baraza linaishauri EWURA:

- i. Kufanya uhakiki wa kina wa vichocheo vikuu vya ongezeko la gharama za O&M katika kipindi cha miaka mitano, hususan ongezeko la takribani asilimia 43.8 kati ya mwaka 2026/27 na 2027/28;
- ii. Kujiridhisha kuwa ongezeko la kila kipengele kikubwa cha gharama linaendana na mabadiliko yanayotarajiwa katika uzalishaji wa maji, idadi ya wateja, ukubwa wa mtandao, matengenezo ya miundombinu na kiwango cha huduma;

- iii. Kuhakiki kwa mahsusi vipengele vinavyoonesha ongezeko kubwa katika kipindi cha Mpango, ikiwemo gharama za umeme kwa uzalishaji wa maji, na kujiridhisha kuhusu sababu na msingi wa makadirio hayo kabla ya gharama hizo kuruhusiwa kurejeshwa kupitia bei;
 - iv. Kuhakikisha kuwa gharama ambazo zinaweza kudhibitiwa kupitia ufanisi wa uendeshaji hazipitishwi moja kwa moja kwa watumiaji bila tathmini ya hatua ambazo Rombo WSSA imechukua kupunguza au kudhibiti gharama hizo; na
 - v. Kuhakikisha kuwa ongezeko la gharama litakaloidhinishwa lineaambatana na maboresho yanayopimika ya huduma, ili watumiaji wapate thamani inayolingana na gharama wanazotarajiwa kubeba.
7. Baraza limepitia malengo ya Rombo WSSA kuhusu upanuzi wa huduma katika kipindi cha Mpango Biashara na kubaini matumizi ya viashiria mbalimbali vya ufikishaji wa huduma ambavyo vinahitaji kufafanuliwa na kuoanishwa ili kuweka wazi kiwango halisi cha huduma kinachotarajiwa kufikiwa na watumiaji katika kipindi cha bei kinachoombewa.

Muhtasari wa Mpango Biashara unaeleza kuwa mojawapo ya malengo ya kimkakati ya Rombo WSSA ni kuongeza wigo wa huduma ya maji kutoka asilimia 63.21 hadi wastani wa asilimia 98 ifikapo Juni 2031. Lengo hilo limerudiwa katika Mpango Kazi wa Mamlaka, ambapo ongezeko la uzalishaji wa maji kutoka mita za ujazo 19,187 kwa siku hadi mita za ujazo 22,902 kwa siku limeainishwa kama mojawapo ya hatua za kufikia lengo hilo (Business Plan, Executive Summary, uk. viii; Jedwali Na. 20, uk. 41).

Hata hivyo, Kiambatisho B-3 cha Mpango Biashara kinatoa ufafanuzi mpana zaidi kwa kutenganisha viashiria viwili vya upatikanaji wa huduma. Kiashiria cha kwanza ni idadi ya watu wanaoishi katika maeneo yaliyofikiwa na mtandao wa maji, ambacho kinatarajiwa kuongezeka kutoka asilimia 63 mwaka 2025/26 hadi asilimia 98 mwaka 2030/31. Kiashiria cha pili ni idadi ya watu wanaohudumiwa kwa maji, ambacho kinatarajiwa

kuongezeka kutoka asilimia 49 mwaka 2025/26 hadi asilimia 65 mwaka 2030/31 (Business Plan, Appendix B-3, uk. 83).

Baraza linaona kuwa viashiria hivyo viwili vinaelezea vipengele tofauti vya huduma. Kufikiwa na mtandao wa maji si sawa na kuhudumiwa kwa maji. Hivyo, asilimia 98 na asilimia 65 hazipaswi kutafsiriwa moja kwa moja kuwa taarifa zinazokinzana. Kwa mtazamo wa mtumiaji, tofauti hii ni muhimu kwa sababu kupanuka kwa mtandao pekee hakumaanishi kwamba wananchi wote waliopo ndani ya eneo hilo watakuwa wameunganishwa au wanapata huduma ya maji.

Kiambatisho hicho kinaonesha zaidi kwamba uwiano wa idadi ya miunganisho ya maji dhidi ya kaya zote unatarajiwa kuongezeka kutoka asilimia 39 mwaka 2025/26 hadi asilimia 56 mwaka 2030/31, huku idadi ya vituo vya kuchotea maji kwa umma ikitarajiwa kuongezeka kutoka 472 hadi 527 katika kipindi hicho. Taarifa hizi zinaonesha umuhimu wa kutofautisha upanuzi wa mtandao na kiwango halisi cha wananchi wanaofikiwa na huduma.

Pamoja na ufafanuzi huo, Baraza limebaini kuwa Sehemu ya 6.2.2 ya Mpango Biashara, inayohusu Mkakati wa Masoko, inaeleza kuwa Rombo WSSA inalenga kuongeza “service coverage” hadi asilimia 86 ifikapo Juni 2031, bila kuweka wazi katika sehemu hiyo kama asilimia 86 inahusu eneo lililofikiwa na mtandao, idadi ya watu wanaohudumiwa au kipimo kingine cha ufikishaji wa huduma (Business Plan, Sehemu ya 6.2.2, uk. 25–26).

Kwa hiyo, hoja ya Baraza si kwamba malengo ya asilimia 98 na asilimia 65 yanakinzana, bali kwamba matumizi ya jumla ya neno “service coverage” katika sehemu mbalimbali za Mpango Biashara yanaweza kuleta tafsiri tofauti kuhusu kiwango cha huduma ambacho Mamlaka inaahidi kukifikia ifikapo mwaka 2030/31. Hali hiyo inaonekana zaidi kutokana na kuwepo kwa lengo jingine la asilimia 86 ambalo halijafafanuliwa kwa namna inayoweza kulinganisha moja kwa moja na viashiria vya Kiambatisho B-3.

Baraza linaona kuwa suala hili lina umuhimu kwa watumiaji kwa sababu mapitio ya bei hayapaswi kuangalia ongezeko la mapato ya Mamlaka pekee, bali pia matokeo ya huduma ambayo mtumiaji anatarajiwa kupata kutokana na bei na uwekezaji

unaoidhinishwa. Malengo yanapaswa kuwa wazi na kupimika ili EWURA na wadau waweze kufuatilia kama ongezeko la bei limeambatana na ongezeko halisi la wananchi wanaopata huduma.

Kutokana na hali hiyo, Baraza linaishauri EWURA:

- i. Kuitaka Rombo WSSA kufafanua na kuoanisha matumizi ya viashiria vya ufikishaji wa huduma katika Mpango Biashara, hususan malengo ya asilimia 98, asilimia 65 na asilimia 86, ili kila kiwango kieleweke kinawakilisha kipimo gani;
 - ii. Kuhakikisha kuwa katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa bei kunakuwa na utofautishaji wa wazi kati ya idadi ya watu wanaoishi katika maeneo yaliyofikiwa na mtandao wa maji na idadi ya watu wanaopata huduma ya maji;
 - iii. Kuweka na kufuatilia malengo ya kila mwaka yanayopimika kuhusu wananchi wanaohudumiwa, miunganisho ya maji, vituo vya kuchotea maji kwa umma na viashiria vingine vinavyoonesha huduma halisi inayomfikia mtumiaji; na
 - iv. Kuhakikisha kuwa utekelezaji wa uwekezaji na ongezeko la bei unaambatana na ongezeko linalothibitishwa la wananchi wanaopata huduma, ili upanuzi wa mtandao uwe na matokeo halisi kwa watumiaji.
8. Baraza limepitia makadirio ya uzalishaji na mahitaji ya maji yaliyowasilishwa na Rombo WSSA na kubaini kuwa Mamlaka bado inakabiliwa na pengo kubwa kati ya kiasi cha maji kinachozalishwa na mahitaji yaliyopo katika eneo lake la huduma.

Mpango Biashara unaonesha kuwa hadi Juni 2025 Rombo WSSA ilikuwa na wastani wa uzalishaji wa takribani mita za ujazo 19,187 kwa siku, ikilinganishwa na mahitaji ya takribani mita za ujazo 34,775.89 kwa siku. Aidha, mahitaji yanatarajiwa kuongezeka hadi mita za ujazo 35,319.36 kwa siku mwaka 2026/27, na kufikia mita za ujazo 37,317.88 kwa siku mwaka 2030/31 (Business Plan, Executive Summary, uk. viii–ix).

Katika kukabiliana na hali hiyo, Rombo WSSA imeweka lengo la kuongeza uzalishaji kutoka mita za ujazo 19,187 kwa siku hadi takribani mita za ujazo 22,902 kwa siku ifikapo Juni 2031. Hatua zinazotarajiwa kuchangia ongezeko hilo ni pamoja na ununuzi na ufungaji wa pampu tatu, ujenzi wa tanki la kuhifadha maji lenye ujazo wa mita za ujazo 2,000 pamoja na uchimbaji na uendelezaji wa visima viwili vipya katika maeneo ya Kiwanda na Mahorosha (Business Plan, Jedwali Na. 19, uk. 39).

Kwa msingi huo, hata baada ya kufikia lengo la uzalishaji wa mita za ujazo 22,902 kwa siku mwaka 2030/31, kiwango hicho kitakuwa bado chini ya mahitaji yanayokadiriwa ya mita za ujazo 37,317.88 kwa siku. Kwa hesabu hiyo, uzalishaji uliolengwa ni takribani asilimia 61.4 ya mahitaji yanayokadiriwa.

Hata hivyo, Baraza linatambua kuwa kulinganisha uzalishaji na mahitaji pekee hakutoi picha kamili ya kiwango cha huduma kitakachopatikana kwa watumiaji. Kama ilivyoelezwa katika Hoja Na. 4 hapo juu, Rombo WSSA pia inalenga kupunguza maji yasiyoingiza mapato kutoka asilimia 67.64 hadi asilimia 25 ifikapo Juni 2031. Kupungua kwa upotevu wa maji kunaweza kuongeza kwa kiasi kikubwa sehemu ya maji yanayozalishwa ambayo hatimaye inapatikana kwa matumizi na kutozwa bili.

Jambo hilo linaonekana pia katika makadirio yaliyotumika kwenye Ombi la Bei. Kiasi cha maji kinachotarajiwa kuzalishwa kinaongezeka kutoka takribani mita za ujazo milioni 7.571 mwaka 2026/27 hadi milioni 8.359 mwaka 2030/31. Wakati huohuo, kutokana pamoja na kupungua kwa NRW kutoka asilimia 50 hadi asilimia 25, kiasi cha maji kinachotarajiwa kutozwa bili kinaongezeka kutoka takribani mita za ujazo milioni 3.785 hadi milioni 6.269.

Hivyo, Baraza linaona kuwa hatua za kuongeza uzalishaji na kupunguza NRW zinapaswa kutazamwa kwa pamoja. Ufanisi katika kupunguza upotevu wa maji unaweza kutoa manufaa makubwa kwa watumiaji hata kama ongezeko la uzalishaji pekee halitoshelezi mahitaji yote yanayokadiriwa.

Pamoja na hilo, pengo linaloendelea kuwepo kati ya uzalishaji na mahitaji linaifanya iwe muhimu kwa Mamlaka kuonesha kwa uwazi namna uwekezaji unaopendekezwa na ongezeko la bei vitakavyotafsiriwa kuwa maboresho halisi ya upatikanaji na uhakika wa huduma kwa watumiaji. Hili ni muhimu zaidi kwa kuwa sehemu ya msingi ya ombi la bei ni kuwezesha Mamlaka kugharamia uendeshaji na uwekezaji unaotarajiwa kuboresha huduma.

Baraza linaona kuwa, mafanikio ya utekelezaji wa bei hayapaswi kupimwa kwa kiasi cha fedha kilichokusanywa au miradi iliyotekelezwa pekee, bali pia kwa matokeo yanayomfikia mtumiaji, ikiwemo kiasi cha maji kinachopatikana, kupungua kwa NRW, muda wa upatikanaji wa huduma na ongezeko la wananchi wanaopata huduma.

Kutokana na hali hiyo, Baraza linaishauri EWURA:

- i. Kujiridhisha kuwa malengo ya kuongeza uzalishaji wa maji kutoka mita za ujazo 19,187 hadi mita za ujazo 22,902 kwa siku yanaungwa mkono na miradi, rasilimali na ratiba halisi za utekelezaji;
- ii. Kuhakikisha kuwa ongezeko la uzalishaji wa maji na upunguzaji wa NRW vinafuatiliwa kwa pamoja kama viashiria muhimu vya matokeo ya bei itakayoidhinishwa;
- iii. Kuitaka Rombo WSSA kuweka na kuripoti malengo ya kila mwaka yanayopimika kuhusu uzalishaji wa maji, NRW, kiasi cha maji kinachofika kwa watumiaji, muda wa upatikanaji wa huduma na idadi ya wananchi wanaopata huduma;
- iv. Kufuatilia utekelezaji wa miradi inayolenga kuongeza uzalishaji na kuboresha miundombinu ili kuhakikisha kuwa fedha zinazopatikana kupitia bei na vyanzo vingine zinatafsirika kuwa maboresho halisi ya huduma; na

v. Kuhakikisha kuwa utekelezaji wa bei katika kipindi cha miaka mitano unaendana na matokeo yanayopimika kwa watumiaji, hususan kuongezeka kwa upatikanaji, uhakika na mwendelezo wa huduma ya maji.

9. Baraza limepitia mpango wa uwekezaji wa Rombo WSSA kwa kipindi cha miaka mitano na kubaini kuwa utekelezaji wa sehemu kubwa ya miradi inayotarajiwa kuboresha huduma unategemea upatikanaji wa ruzuku kutoka Serikalini na vyanzo vingine vya nje.

Mpango Biashara unaonesha kuwa Rombo WSSA inatarajia kufanya uwekezaji wa jumla wa takribani Shilingi bilioni 44.093 katika kipindi cha mwaka 2026/27 hadi 2030/31. Kati ya fedha hizo, takribani Shilingi bilioni 10.349 zinatarajiwa kutoka vyanzo vya ndani vya Mamlaka, wakati takribani Shilingi bilioni 33.744 zinatarajiwa kutoka katika ruzuku za Serikali. Hii ina maana kuwa takribani asilimia 76.5 ya uwekezaji wote uliopangwa unategemea ruzuku (Business Plan, Executive Summary, uk. ix).

Kwa mwaka mmoja mmoja, ruzuku zinazotarajiwa ni takribani Shilingi bilioni 4.987 mwaka 2026/27, bilioni 6.651 mwaka 2027/28, bilioni 11.820 mwaka 2028/29, bilioni 6.085 mwaka 2029/30 na bilioni 4.200 mwaka 2030/31. Hivyo, utekelezaji wa sehemu kubwa ya mpango wa uwekezaji unategemea fedha hizo kupatikana kwa kiwango na muda uliopangwa.

Ombi la Mapitio ya Bei lenyewe linathibitisha utegemezi huo kwa kueleza kuwa Rombo WSSA imeainisha Serikali kupitia Wizara ya Maji pamoja na washirika wa maendeleo kama vyanzo vingine vya fedha za uwekezaji, ambavyo vinatarajiwa kugharamia zaidi ya asilimia 80 ya gharama za uwekezaji (Tariff Application, Sehemu ya 16).

Baraza linatambua kuwa matumizi ya ruzuku katika kugharamia miradi mikubwa ya maji yana manufaa kwa watumiaji, kwa kuwa yanawezesha utekelezaji wa uwekezaji ambao ungekuwa mgumu kugharamiwa kupitia mapato ya Mamlaka pekee. Kwa hiyo, utegemezi wa ruzuku si tatizo kwa wenyewe. Jambo la msingi ni kuhakikisha kuwa utekelezaji wa maboresho ya huduma yaliyoahidiwa katika kipindi cha bei hauathiriki kwa kiasi kikubwa endapo fedha hizo hazitapatikana kwa wakati au kwa kiwango kilichotarajiwa.

Umuhimu wa jambo hili unatambuliwa pia na Rombo WSSA yenyewe. Katika uchambuzi wa vihatarishi, Mpango Biashara umetaja utegemezi mkubwa wa fedha kutoka nje kwa ajili ya uwekezaji mkubwa kuwa mojawapo ya vihatarishi vikuu vya utekelezaji. Hatua zilizopendekezwa kukabiliana na kihatarishi hicho ni pamoja na kuongeza mapato ya ndani kupitia ongezeko la wateja, kutafuta mikopo yenye masharti nafuu, kushirikisha sekta binafsi na kuongeza juhudi za kupata fedha kutoka kwa taasisi zinazofadhili miradi (Business Plan, Executive Summary, Major Risks and Mitigation Measures).

Aidha, katika uchambuzi wa mazingira ya nje, Mpango Biashara unatambua kuwa kukosekana kwa fedha kutoka nje kunaweza kuifanya Mamlaka ishindwe kutekeleza uwekezaji mkubwa, na Rombo WSSA imeeleza kuwa itatafuta fedha kutoka Serikalini na washirika wengine wa maendeleo kwa ajili ya miradi mikubwa na ya kimkakati.

Jambo hili lina umuhimu wa moja kwa moja kwa watumiaji kwa sababu baadhi ya malengo muhimu ya huduma yanategemea uwekezaji huo. Kwa mfano, Mpango Kazi unaonesha kuwa hatua za kuongeza uzalishaji kutoka mita za ujazo 19,187 hadi 22,902 kwa siku, ikiwemo ununuzi na ufungaji wa pampu na ujenzi wa tanki la mita za ujazo 2,000, zimepangwa kutekelezwa kwa kiasi kikubwa kupitia ruzuku (Business Plan, Jedwali Na. 20, uk. 41).

Kwa hiyo, endapo ruzuku zilizopangwa zitachelewa au hazitapatikana kwa kiwango kilichotarajiwa, kuna uwezekano wa kuchelewa kwa baadhi ya miradi na, kwa sababu hiyo, maboresho ya huduma yaliyotarajiwa na watumiaji yanaweza pia kuchelewa. Kwa mtazamo wa Baraza, jambo hilo linahitaji kuzingatiwa katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa bei ili watumiaji wasipimwe kwa matarajio ya maboresho ambayo utekelezaji wake umechelewa kutokana na kutopatikana kwa fedha za uwekezaji.

Kutokana na hali hiyo, Baraza linaishauri EWURA:

- i. Kujiridhisha kuhusu hali ya upatikanaji na uhakika wa vyanzo vya ruzuku vilivyotumika katika Mpango wa Uwekezaji wa Rombo WSSA, hususan kwa miradi mikubwa inayotarajiwa kuleta maboresho ya moja kwa moja ya huduma;
- ii. Kuitaka Rombo WSSA kuweka na kuripoti kwa kila mwaka taarifa kuhusu ruzuku zilizopangwa, kiasi kilichopatikana, miradi iliyotekelezwa na matokeo ya huduma yaliyopatikana;
- iii. Kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa miradi inayotegemea ruzuku na athari za ucheleweshaji au kutopatikana kwa fedha hizo katika kufikia malengo ya uzalishaji, wigo wa huduma, kupunguza NRW na kuboresha upatikanaji wa maji;
- iv. Kuitaka Rombo WSSA kuwa na mpango mahsusi wa kukabiliana na upungufu au ucheleweshaji wa fedha za nje, ukiweka vipaumbele katika miradi yenye manufaa makubwa na ya moja kwa moja kwa watumiaji; na
- v. Kuhakikisha kuwa katika ufuatiliaji wa bei na utendaji wa Mamlaka, uwekezaji unaotarajiwa unatofautishwa na uwekezaji uliotekelezwa, na maboresho ya huduma yanatathminiwa kwa kuzingatia miradi na rasilimali zilizopatikana na kutumika katika kipindi husika.

10. Kwa kuzingatia uchambuzi wa Ombi la Mapitio ya Bei la Rombo WSSA, Mpango Biashara wa miaka mitano pamoja na nyaraka nyingine zilizowasilishwa, Baraza linatambua umuhimu wa Mamlaka kuwa na mapato ya kutosha kugharamia uendeshaji na matengenezo ya huduma, kutekeleza uwekezaji unaohitajika na kuhakikisha uendeleu wa huduma ya maji.

Aidha, Baraza linatambua changamoto zinazoikabili Rombo WSSA, ikiwemo kiwango kikubwa cha maji yasiyoingiza mapato, pengo kati ya uzalishaji na mahitaji ya maji, miundombinu inayohitaji ukarabati, pamoja na mahitaji ya kuongeza wigo na uhakika wa huduma. Nyaraka za Mamlaka zinaonesha, kwa mfano, kuwa NRW ilikuwa asilimia 67.64 na inalengwa kupungua hadi asilimia 25, wakati uzalishaji wa maji wa takribani mita za

ujazo 19,187 kwa siku unatarajiwa kuongezeka hadi mita za ujazo 22,902 kwa siku ifikapo Juni 2031.

Baraza pia linatambua kuwa utekelezaji wa Mpango Biashara unahitaji uwekezaji mkubwa. Rombo WSSA imepanga uwekezaji wa takribani Shilingi bilioni 44.093, ambapo sehemu kubwa, takribani Shilingi bilioni 33.744, inatarajiwa kugharamiwa kupitia ruzuku za Serikali.

Hata hivyo, katika kufanya uamuzi kuhusu ombi la bei, Baraza linaona umuhimu wa kuweka uwiano kati ya uendeleu wa kifedha wa Mamlaka na ulinzi wa maslahi ya watumiaji. Bei inayolipwa na mtumiaji inapaswa kutokana na gharama za lazima, halali na zenye ufanisi, na ongezeko lolote la gharama kwa mtumiaji linapaswa kuambatana na maboresho yanayopimika ya huduma.

Kwa msingi huo, Baraza linaomba EWURA, wakati wa kufanya uamuzi kuhusu ombi la Rombo WSSA, izingatie kwa pamoja mambo yafuatayo:

- i. Uhalisia na uoanifu wa bei inayoombwa, hususan tofauti iliyobainika katika kiwango cha wastani cha bei ya mwaka 2026/27, ili bei itakayoidhinishwa iwe na msingi mmoja unaoeleweka na kuthibitishwa;
- ii. Uwezo wa watumiaji kumudu huduma, hususan kutokana na ongezeko kubwa la wastani wa bei linalojitokeza katika miaka ya mwanzo ya kipindi cha bei;
- iii. Uhalali na ufanisi wa gharama zinazorejeshwa kupitia bei, hususan ongezeko la gharama za uendeshaji na matengenezo, ili watumiaji wasibebeshwe gharama zinazoweza kuepukwa kupitia ufanisi wa Mamlaka;
- iv. Utekelezaji wa mpango wa kupunguza maji yasiyoingiza mapato, kwa kuwa makadirio ya bei na mapato yamejengwa kwa msingi wa kupungua kwa NRW kutoka asilimia 50 mwaka 2026/27 hadi asilimia 25 mwaka 2030/31;

- v. Uhakiki wa Msingi wa Mali Unaodhibitiwa (RAB) na Marejesho ya Uwekezaji (ROI), ikiwemo kuhakikisha kuwa mali zinazofadhiliwa kwa ruzuku zinatambuliwa na kushughulikiwa ipasavyo katika ukokotoaji wa marejesho yanayorejeshwa kupitia bei;
- vi. Uwazi na uoanifu wa malengo ya huduma, kwa kutofautisha kwa uwazi upanuzi wa mtandao wa maji na idadi halisi ya wananchi wanaopata huduma, ili mafanikio ya utekelezaji yaweze kupimwa kwa matokeo yanayomfikia mtumiaji;
- vii. Uoanifu kati ya uzalishaji, mahitaji ya maji na hatua za kupunguza NRW, ili ongezeko la bei na uwekezaji unaotekelezwa viweze kutafsiriwa kuwa ongezeko la upatikanaji, uhakika na mwendelezo wa huduma; na
- viii. Uhakika wa utekelezaji wa miradi inayotegemea ruzuku, kwa kuzingatia kuwa sehemu kubwa ya uwekezaji uliopangwa inategemea fedha kutoka Serikalini na vyanzo vingine vya nje, na kwamba Rombo WSSA yenyewe imetambua utegemezi mkubwa wa fedha za nje kuwa mojawapo ya vihatarishi vya utekelezaji wa Mpango Biashara.

Baraza linaona kuwa, mambo hayo yanapaswa kutazamwa kwa pamoja ili uamuzi wa bei uweze kuwezesha Rombo WSSA kuendelea kutoa huduma endelevu bila kuhamishia kwa watumiaji gharama zisizo za lazima au zisizo na ufanisi, na wakati huohuo kuhakikisha kuwa ongezeko la bei linaambatana na maboresho halisi ya huduma.

11. Baraza linatambua umuhimu wa Rombo WSSA kuwa na uwezo wa kifedha wa kugharamia uendeshaji na matengenezo ya huduma, kufanya uwekezaji unaohitajika, kupunguza maji yasiyoingiza mapato, kuongeza uzalishaji na kupanua huduma kwa wananchi wa Wilaya ya Rombo. Ombi la mapitio ya bei linapaswa, kwa hiyo, kutazamwa kwa kuzingatia mahitaji ya uendelevu wa Mamlaka pamoja na haki na maslahi ya watumiaji.

Baraza pia linatambua kuwa Rombo WSSA imeweka malengo ya kuboresha huduma katika kipindi cha miaka mitano, yakiwemo kupunguza NRW hadi asilimia 25, kuongeza uzalishaji wa maji hadi takribani mita za ujazo 22,902 kwa siku na kufanya uwekezaji katika miundombinu ya maji.

Hata hivyo, uchambuzi wa Baraza umebainisha maeneo yanayohitaji EWURA kujiridhisha zaidi kabla na wakati wa utekelezaji wa bei, yakiwemo uoanifu wa bei inayopendekezwa, uwezo wa watumiaji kumudu ongezeko la bei, uhalali na ufanisi wa gharama, kupungua kwa NRW, uhakiki wa RAB na ROI, uwazi wa malengo ya huduma, pamoja na utekelezaji wa miradi inayotegemea ruzuku.

Kwa msingi huo, Baraza linaishauri EWURA kufanya tathmini ya kina ya ombi la Rombo WSSA kwa kuzingatia uendelevu wa huduma, ufanisi wa gharama, uwezo wa watumiaji kumudu bei na maboresho yanayotarajiwa ya huduma, na kuhakikisha kuwa gharama zitakazoruhusiwa kurejeshwa kupitia bei ni zile tu zilizothibitishwa kuwa za lazima, halali na zenye ufanisi.

Aidha, Baraza linasisitiza umuhimu wa bei itakayoidhinishwa kuambatana na malengo ya kila mwaka yanayopimika na kufuatiliwa, hususan kuhusu uzalishaji wa maji, kiwango cha NRW, muda wa upatikanaji wa maji, idadi ya wananchi wanaopata huduma na utekelezaji wa miradi ya uwekezaji.

Kwa kufanya hivyo, uamuzi wa bei utaweka uwiano unaohitajika kati ya uwezo wa Rombo WSSA kutoa huduma endelevu na yenye ubora na wajibu wa kumlinda mtumiaji dhidi ya gharama zisizo za lazima, huku ukihakikisha kuwa ongezeko la gharama analobeba mtumiaji linaendana na thamani na maboresho halisi ya huduma anayopokea.

Naomba kuwasilisha.